
# Usimamizi mbovu katika vipimo unawagharimu wakulima nchini




Mwandishi Wetu, Mwananchi

Usimamizi mbovu wa kuhakikisha vipimo sahihi vinavyotumika katika biashara ndiyo unasababisha wakulima kupata hasara baada ya kulanguliwa mazao yao na wafanyabiashara wasio waaminifu kabla ya baada ya mavuno.

Pamoja na kuwapo kwa sheria ya vipimo, hakuna ufuatiliaji na utekelezaji wa sheria hiyo jambo linalowakwamisha wakulima kuboresha kilimo chao na baadhi yao kuzidi kukithiri kwa maskini.

Chama cha Wafanyabiashara wenye viwanda na kilimo (TCCIA) tawi la Iringa katika ripoti yake, pamoja na kuwapo na juhudi kubwa za mamlaka husika kukabili vipimo feki kama lumbesa, vipimo hivyo bado ni kikwazo kwa wakulima.

Mwenyekiti wa TCCIA Iringa, Lucas Mwakabungu anasema kipimo cha lumbesa ni moja ya mambo 10 wanataka kuyashughulikia kwa kuwa yanaharibu mazingira ya biashara, kuvuruga kilimo na kumnyonya mkulima.

Anasema: "Tija katika kilimo ni ndogo kutokana na changamoto nyingi zinazowakabili wakulima."

Anasisitiza kwamba, wakati umefika wa kuboresha mazingira ya biashara ili kuongeza pato la wakazi wa Iringa na Taifa.

Anasema kama suala hilo litashughulikiwa katika sekta ya kilimo hasa kwenye vipimo, ni dhahiri pato la Taifa litaongezeka na kukuza fursa za ajira.

**Hasara ya Sh174 bilioni**

Mwakabungu anasema katika utafiti uliofanywa miaka miwili iliyopita, ilibainika kwamba kwa mtindo huo wa lumbesa, wakulima wa Njombe na Iringa wanapoteza zaidi ya Sh14.7 bilioni kwa mwaka baada ya kuuza mazao yao kwa wafanyabiashara wasiowaaminifu.

"Kwa kutumia takwimu hizo hizo na kwa mazingira yanayofanana, kiasi cha thamani cha mahindi na mpunga kinachopotea kwa nchi nzima kwa sababu ya vipimo vya lumbesa ni takriban Sh14.8 bilioni na wakulima wanapoteza wastani wa Sh174 bilioni kwa mwaka," inasema ripoti ya utafiti huo.

Tangu kutolewa kwa utafiti huo, hakuna mabadiliko makubwa ya msingi yaliyotokea kukabiliana na athari za lumbesa.

**Lumbesa ni kipimo haramu**

Sheria ya vipimo namba 20 ya mwaka 1984, inawataka wananchi kuheshimu vipimo halali katika biashara zao. Sheria ya Vipimo ya mwaka 1982 na mabadiliko yaliyofuatia, inaweka wazi namna bidhaa za kilimo zinavyopaswa kuuzwa. Kimsingi, kuna kiwango maalumu cha ujazo kinachotakiwa kwa kila kifungashio kinachohusika.

Matumizi ya vipimo ambavyo havijasajiliwa na vyenye ujazo kinyume kama lumbesa wakati wa kununua mazao ya wakulima, kumezuiliwa kisheria lakini katika maeneo mengi imekuwa kama kawaida matumizi hayo kufanyika. Na hali huwa mbaya zaidi kama wakulima wanauza mazao yao moja kwa moja wakiwa shambani.

Ingawa mara zote Serikali inasema kipimo cha lumbesa kisiruhusiwe kutumika, bado utaratibu wa kukazia sheria hiyo umebaki kuwa changamoto kubwa.

**Wakala wa vipimo**

Wakala wa Vipimo (WMA), ambao unafanya kazi hii kwa miongo mitano sasa, ndicho chombo kinachotakiwa kuhakikisha kwamba sheria katika mazingira yote kuhusiana na vipimo inatekelezwa.

Tafiti mbalimbali zilizofanyika zinaonyesha kwamba WMA haina uwezo wa kuhakikisha kwamba sheria zilizopo kuhusu vipimo zinatekelezwa kutokana na changamoto mbalimbali zikiwamo za kiutendaji na ukosefu wa fedha. Hali inakuwa mbaya zaidi mkulima anapouza bidhaa zake kwa mtu wa kati, wakala au akiwa shambani.

Mathalan kwa upande wa Iringa kuna watu zaidi ya milioni 1.5 wanaohitaji huduma za vipimo, ofisi za WMA ambazo zinatakiwa kuhudumia watu hao, ofisi yao ya Iringa ina wafanyakazi watatu. Maana yake, pamoja na kuwapo kwa uelewa kuhusu lumbesa, uwezekano wa kukabiliana vikali na desturi hiyo ni mdogo.

Katika hili TCCIA inaitaka Serikali kutumia mfumo shirikishi wa kuwezesha utekelezaji wa sheria ya vipimo kwa kushawishi na kuwaingiza wadau zaidi katika kuhakikisha kwamba sheria ya vipimo inatekelezwa.

**Changamoto 10 zinazokaibili sekta ya kilimo Iringa**

Ukiwa mkoa muhimu kwa kilimo, Iringa unakabiliwa na changamoto zifuatazo;

Bei kubwa ya pembejeo kama mbolea, dawa za kuulia wadudu au magugu, mbegu na mengineyo.

Pia, kuwapo kwa mfumo wa soko huru unaowafanya wafanyabiashara wasio waadilifu kuingiza pembejeo feki kama mbolea na mbegu zilizo chini ya viwango.

Vilevile, mazao kukosa mnyororo wa thamani. Hakuna viwanda vya kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa na mkulima ili kuwa na soko pana zaidi.

Gharama kubwa za nishati kama vile umeme.

Ukosefu wa mitaji kwa ajili ya kuwekeza katika viwanda vya kilimo na kukosekana kwa uwezo wa kurejesha mkopo.

Kushindikana kwa matumizi ya vipimo kwa mujibu wa Sheria ya Vipimo ya mwaka 1982 na kuzagaa kwa matumizi ya vipimo feki kama lumbesa kumesababisha wakulima kupata hasara.

Hakuna soko la uhakika na wakulima wanaweza kuuza mazao yao.

Kutokuwa na bei inayoeleweka ya mazao ya kilimo.

Ubovu wa miundombinu ya barabara za vijijini ambako kuna wakulima.

Kutokuwapo kwa ardhi iliyopimwa na kutengwa kwa ajili ya wawekezaji.

***Kwa maoni kuhusiana na uboreshaji wa mazingira ya biashara nchini Tanzania tuma ujumbe mfupi (SMS) kwa 0786240172. Maelezo yako yanathaminiwa sana na yakichapishwa katika gazeti utapewa muda wa maongezi wa sh elfu 30.***

**SAUTI ZA WANANCHI**

**Christinsa Geleja:**

**Kuna tatizo la kodi ambalo linaleta kikwazo katika kufanya biashara. Serikali imeendelea kuongeza kodi kwa wenye shughuli rasmi, lakini wakiacha kuwatoza kodi wale ambao wanaendesha shughuli za kiuchumi ambazo si rasmi na hawajasajili.**

**Kutokana na kutohangaika na hao wengine, walio katika sekta rasmi wamekuwa wakibebeshwa mzigo wa kodi. Ni vema Serikali ikahakikisha kwamba kila shughuli ya kiuchumi inayotoa kipato inatozwa kodi.**

**Octavina Mtei, Morogoro**

**Ili kuboresha mazingira ya biashara, ni lazima Serikali ifikirie kupunguza kodi na tozo mbalimbali. Kama inawezekana wenye viwanda vidogo wasitozwe kodi wala ushuru. Wenye biashara ndogo wanalazimishwa kununua mashine za kielektroniki (EFDs) zinazogharimu Sh70,000 huku mtu huyo akiwa na mtaji wa kujiendesha wa pengine Sh1 milioni. Katika mazingira hayo mtu anawezaje kutengeneza faida?**

**Katika hali ya kawaida sehemu kubwa ya kodi zilitakiwa kulipwa na wafanyabiashara wakubwa na katika hili EFDs inastahili kuwa kwa wafanyabiashara wakubwa.**

UKURASA HUU UMEDHAMINIWA NA
BEST-Dialogue
Doing business, let's make it easy - and fair
Kufanya biashara kwa haki - bila vikwazo